Umepewa dakika 40 kuandika insha yako.

***Andika hotuba uliyotoa kuhusu umuhimu wa kudumisha amani nchini Kenya.***

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

__1__. Ni vigumu__2__mazingira yetu bila ya kuwa na elimu. Kutokana na ukweli huu wazazi wengi wamepeleka watoto wao shuleni ili__3__ waweze kujikimu. Elimu __4__ kila mtoto msingi__5__ wa kuweza kujitegemea maishani__6__. Kwanza kukidhi mahitaji yake, yaani __7__. Hili nalo__8__kuwatia ari ya kuweza kuendelea

1. **A.** Elimu bila amali kama nta bila asali **B.** Elimu ni mali ambayo adui hawezi kuiteka **C.** Elimu ni taa, gizani huzagaa **D.** Elimu maisha si vitabu
2. **A.** kuzimudu **B.** kuyamudu **C.** kuimudu **D.** kulimudu
3. **A.** siku za kisogoni **B.** siku za halafu **C.**siku za mambo **D.** siku za kinyama
4. **A.** hukupa **B.** huwapa **C.** hunipa **D.** humpa
5. **A.** bora **B.** vizuri **C.** uthabiti **D.** wema
6. **A.** yake **B.** mwangu **C.** mwake **D.** mwako
7. **A.** kujitosheleza **B.** kujiweza **C.** kujijali **D.** kujitunza
8. **A.** inaweza **B.** linaweza **C.** unaweza **D.** kumtia

Aidha mtoto hujifunza __9__ muhimu, kama vile huruma, upendo, ushirikiano na ukarimu __10__ huchangia kuwepo kwa jamii thabiti. Hapa mtoto huhimizwa kushirikiana na wenzake kama__11__. Mwana akiwa shuleni vipawa vyake__12__. Hivi vinaweza kuwa chanzo cha kupata jina baadaye. Shule moja huwa na wanafunzi kutoka __13__mbalimbali za taifa ambao husoma pamoja __14__ huweza kuimarisha__15__ wa kitaifa.

9. **A.** maadili **B.** stadi **C.** maarifa **D.** masomo
10. **A.** ambazo **B.** ambao **C.** ambayo **D.** ambavyo
11. **A.** chanda na pete **B.** jicho na kidole **C.** ardhi na mbingu **D.** kiko na digali
12. **A.** hugunduliwa na kuhifadhiwa **B.** huonekana na kuvumbuliwa **C.** hutarajiwa na kupendekezwa **D.** hutambuliwa na kukuzwa
13. **A.** eneo **B.** janibu **C.** maeneo **D.** upande
14. **A.** : **B.** ? **C.** ; **D.** /
15. **A.** utangamano **B.** utegemezi **C.** utengano **D.** utandawazi

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** Andika udogo wa sentensi ifuatayo: Nyumba hiyo ilijengwa kwenye mlima ule
- A. Kinyumba hicho kilijengwa kwenye kilima kile
- B. Kijumba hicho kilijengwa kwenye mlima ule
- C. Kijumba hicho kilijengwa kwenye kilima kile
- D. Jumba hilo lilijengwa kwenye lima lile

**17.** **Kanusha sentensi ifuatayo:** *Mgeni alipofika alimpata mwenyeji wake.*
- A. Mgeni hakufika wala kumpata mwenyeji wake.
- B. Mgeni alipofika hakumpata mwenyeji wake.
- C. Mgeni alifika ingawa hakumpata mwenyeji wake
- D. Mgeni asipofika huwa hampati mwenyeji wake

**18.** Gonjera ni nini? Ni shairi-:
- A. lililo na vina vinavyobadilika badilika katika ubeti.
- B. linalokaririwa na watu wawili au zaidi kwa kujibizana.
- C. lililo na mshororo wa mwisho ambao unarudiwarudiwa
- D. linalosimulia tukio fulani na huwa na kipande kimoja

**19.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi
- A. Mtu huyu ni fisadi lakini yule ni mwadilifu
- B. Maskanini mwangu mmenadhifishwa na kitwana
- C. Gari la kwanza limefika kwenye stani mapema.
- D. Mgeni atawasili mnamo saa saba adhuhuri

**20.** **Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo.** *"Andikeni kazi hiyo katika vitabu vyenu," Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa...........*
- A. Mwalimu aliwaambia wanafunzi kuwa wangeandika kazi hiyo katika vitabu vyao.
- B. Mwalimu aliwaambia waandike kazi hiyo katika vitabu vyenu.
- C. Mwalimu aliwahimiza wawe wakiandika kazi ile katika vitabu vyao.
- D. Mwalimu aliwaagiza kuifanya kazi hiyo katika vitabu vyao.

**21.** **Chagua sentensi yenye -kwa- inayoonyesha 'pamoja na'.**
- A. Sema alipendwa kwa heshima yake
- B. Tulienda moja kwa moja hadi uwanjani
- C. Wake kwa waume walishiriki sherehe hiyo
- D. Nuru alipata alama saba kwa kumi

**22.** Chagua jozi ya methali zenye maana kinyume:

*(i) Kuku havunji yai lake.*
*(ii) Damu ni nzito kuliko maji*
*(iii) Ibilisi wa mtu ni mtu*
*(iv) Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.*

| | |
|---|---|
| A. (i), (ii) | B. (iv), (v) |
| C. (i), (iii) | D. (i), (iv) |

**23.** Tambulisha sentensi iliyoakifishwa vizuri.
- A. Darasa hili, "akasema," Lina wanafunzi watiifu."
- B. "Darasa hili, "akasema," lina wanafunzi watiifu."
- C. "Darasa hili," akasema, "lina wanafunzi watiifu."
- D. "Darasa hili," akasema, "Lina wanafunzi watiifu."

**24.** Nomino **chai, sukari na asali** huorodheshwa katika ngeli ipi?

| | |
|---|---|
| A. I - I | B. I - ZI |
| C. U - Zi | D. U - YA |

**25.** **Badilisha sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendwa:** *Omari alienda mtoni akayachota maji ya nyanya*
- A. Maji ya nyanya yalichotwa mtoni na Omari.
- B. Omari alimchotea nyanya maji yake mtoni
- C. Mtoni kulichotwa maji ya nyanya na Omari
- D. Nyanya alichotewa maji mtoni na Omari



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**26.** Kutokana na sifa aminifu, tunapata nomino gani?

A. Amini B. Uaminifu
C. Aminika D. Amani

**27.** Arbuni ni

A. sehemu ya bei ya kitu inayotolewa mwanzoni
B. sehemu ya ujira wa kumsaidia mtu mwanzoni
C. sehemu ya fidia anayolipwa mtu mwanzoni
D. sehemu ya malipo ya kukopea kitu mwanzoni

**28.** Chagua sentensi iliyotumia kihisishi kifaacho.

A. Shabash! Majambazi hao waliwajeruhi wenyeji
B. Ole wangu! Matokeo haya ni mazuri ajabu
C. Pepa! Umeiletea timu yetu sifa bora
D. Inshalla! Tulifika salama salmini

**29.** **Ni sentensi ipi iliyotumia -ingine- kuonyesha 'badala ya'?**

A. Raia wengine hupenda kulinda usalama
B. Juma alituambia hadithi nyingine ya kuvutia
C. Watalii wengine wanatarajiwa kesho asubuhi
D. Menza anahitaji nguo nyingine, hii haimpendezi

**30.** Chagua sentensi ambayo inaunganisha sentensi zifuatazo ipasavyo

Gari lilikuwa jipya. Gari halikumpendeza:

A. Gari lilikuwa jipya madhali halikumpendeza
B. Licha ya gari kuwa jipya halikumpendeza
C. Gari lilikuwa jipya angaa halikumpendeza
D. Mithili ya gari kuwa jipya halikumpendeza

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.</u>***

Kaza alikuwa kijana aliyeenziwa na hata alipokuwa katika shule ya upili. Kila mmoja alimtaka mtoto wake afanye bidii kama Kaza. Nakumbuka alipokivuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya Bidii. Azma yake ilikuwa kusoma kwa bidii ili kuinuka kwa kijana wa kutegemewa na jamii yake. Familia yao haikuwa tajiri aidha haingeitwa maskini.Alisoma kwa bidii za wazazi wake jambo ambalo lilimwezesha kukwangura alama za kumezewa mate. Kaza alijua kuwa hata akiwa shule ya upili bado alikuwa mwanafunzi chini ya wazazi wake. Hata katika maisha ya mahali shule hii ya Bidii ilipopatikana. Kwa kweli hii ndiyo iliyokuwa mara yake ya kwanza kutia guu kwenye jiji hili ambalo habari zake akizisoma, ama katika magazeti machache yaliyowahi kufika kijijini mwao au kupitia somo la Elimujamii. Hata hivyo kama tu jina lake, Kaza hakuwa mtu wa kuogopa au kunywea machoni mwa changamoto.

Baada ya kujikaza kisabuni, Kaza aliweza kufanya bidii na kupita japo alama zake hazikumwezesha kujiunga na chuo kikuu. Hapo ndipo alipoamua kugunia mjini badala ya kujikalia nyumbani bila shughuli zozote. Si wajua kwenda bure si kukaa bure?

Mjini alipata kibarua cha kuburura rukwama. Kazi hii aliifanya kutwa, katika masoko na vichochoro vya mji huku akiwabebea watu mizigo kwa malipo ya kijungumeko. Pesa kichele alizoambulia ndizo zilizomwezesha kumudu uraibu wake wa pombe hatari, kulipia chumba kimoja alichopanga kwenye mtaa wa mabanda na kugharamia chakula chake ambacho bila shaka unaweza kutabiri hali yake. Kila jioni alijiunga na watu kufu yake kupiga ugimbi na starehe nyingine ambazo wangemudu.

Mara nyingi Kaza na wenzake hawa walijipata wameangukia mikononi mwa walinda usalama. Hapo ndipo waliweza kusombwa mithili ya taka na kutiwa kwenye malori yaliyowapeleka kwenye seli mbalimbali. Hapo walioweza kutoa kinyegezi wangefanya hivyo na kununua uhuru wao. **<u>Ole wao ambao walijitia kuchanikiwa na vibindo</u>**. Wangerambishwa mateke ya kila aina na kutundikwa ndani hadi wakati ambapo wangepata msamaria mwema wa kuja kuwatoa humo kwa dhamana ambayo iliishia mikononi mwa walinda haki na vituo vya polisi.

**Shida za mji zilimguguna na kufanya mambo yake yaende mvange.** Kaza akaona hali ngumu katika mji huu wa Umayamaya wa watu. Hakuwa ameyazoea maisha haya ya kuchanika kwenye mpini. Kila mara na kulalia mate wakati huo huo. Aliishi na wenzake ambao tayari walikuwa wamezizoea vitimbi vya mji. Wao walimudu ulevi kila siku na kupata fulusi za kuwapenyezea wenye macho mapekuzi. Hata hivyo hali ya Kaza haikuwa ya kuridhisha. Dhomba za mji zilimpiga yeye maradufu ya vijana wenzake. Je hawakusema wasemao kuwa baridi humzizima kondoo mwenye manyoa haba. Kaza alikuwa mwanagenzi katika maisha ya mji na daima mwanagenzi huwa na mengi ya kujutia.

Nakumbuka siku hiyo kama kwamba ilikuwa jana. ilikuwa ijumaa moja usiku wa manane. Kaza aliamshwa na vishindo vya watu na sauti ya magari. Alichungulia kwenye tundu aliloita dirisha la chumba chake na kukumbana na mianga mikali ya matingamatinga yaliyokuwa yakijiendea tu bila kujali kuwa yalikuwa yakipitia juu ya nyumba za maskini hawa.

Kaza hakuwa na la kufanya ila kujiangalilia kwa jitimai ya kudunisha nafsi vibanda vya majirani vikinywea na kuanguka chini kutokana na shinikizo la msema kweli huyu. Alielewa kuwa wakati wa kuondoa kidogo alichokuwa nacho ulikuwa umewadia. Alijizoazoa na kwanza kukusanya milki yake ya pekee aliyokuwa nayo. Hata kabla ya kunyanyua chochote, alisikia sauti kali ikimwambia atoke kabla ya kuwa kima. Kaza akatii amri shingo upande. Akachukua furushi lililojaa magwanda yake ya kazi na kutoka. Tingatinga halikuchelewa kukilainisha kibanda chake na kukumbusha kuwa maisha yake na wenzake yalikuwa yamechukua mkondo mpya.

Upepo na baridi yabisi ya asubuhi ilimpata kaza amejishika tama mbele ya kilichokuwa kibanda chake. Hakujua kwa nini kaandamwa na nuksi ya aina hiyo. Alipowasili wenzake kisa na maana ya hayo yote, aliambiwa kuwa hiyo ilikuwa shughuli ya kidesturi ya serikali kuusafisha mji na kupunguza ombaomba katika mitaa iliyopakana na mitaa ya kifahari. Ingawa Kaza alikuwa kakatika maini wenzake hawakuonekana kupigwa na mshipa. Walisema wangengoja siku mbili - tatu chura hao wasahau kisha warudi kuvijenga vibanda vyao. Kaza alijiona kama nyumba ya udongo isiyoweza kumihili vishindo. Moyo wake ulimuasa kuwa yeye alikuwa jogoo la shamba na tangu hapo jogoo la shamba haliwiki mjini. **Aliamua kufunganya virago vyake na kurudi nyumbani kushika jembe.**

**31.** Chagua kauli ya kweli kulingana na aya ya kwanza?

A. Nia ya Kaza katika elimu ilikuwa kuinua hali ya familia yake.
B. Nia ya Kaza katika elimu ilikuwa kuisaidia jamii yake.
C. Nia ya Kaza katika elimu ilikuwa kupata alama nzuri
D. Nia ya Kaza katika elimu ilikuwa kujiunga na shule ya Bidii

**32.** Kaza alipojiunga na shule ya Bidii,

A. alifahamu machache kuhusu wanagenzi
B. alijua machache kuhusu masomo ya shule ya Bidii
C. alifahamu machache kuhusu jiji ambalo shule ilipatikana
D. alijua machache kuhusu maisha mapya

**33.** Idara za usalama kwa mujibu wa kifungu hiki

A. zinapinga uuzaji wa pombe haramu mjini
B. zinawadhulumu wanyonge haki zao kazini
C. zinapinga hali ya watu kuishi maisha hatari
D. zinaendeleza ufisadi badala ya mkondo wa haki

**34.** Jambo ambalo Kaza hakuzoea ni.

A. kujifanyia mambo mengi maishani mwake
B. kukabiliana na walinda usalama mara kwa mara
C. kufanya bidii sana ilhali kipato ni duni
D. kutumia mihadarati na ukosefu wa chakula.

**35.** Ni nini maana ya kauli hii:
**<u>Ole wao ambao walijitia kuchanikiwa na vibindo.</u>**

A. Walionekana kuishi maisha ya kufanya kazi ya kijungumeko
B. Waliokosa pesa za kununua uhuru wao
C. Walioshindwa kutambua mbinu mwafaka ya kununua uhuru wao
D. Waliofanya kuwa hawakuelewa kile maafisa wa polisi walikuwa wakitaka.

**36.** Lengo la ubomoaji wa vibanda ni kuwa,

A. vilishusha hadhi ya maeneo ya matajiri
B. vilihatarisha maisha ya wote waliokuwa matajiri wa karibu na mbali
C. viliwahifadhi wahuni waliohatarisha usalama wa mabwanyenye jirani
D. vilijengwa katika ardhi iliyomilikiwa na serikali.

**37.** Tambua tamathali mbili za lugha zinazopatikana katika kauli hii:
**<u>Shida za mji zilimguguna na kufanya mambo yake yaende mvange.</u>**

A. Tashhisi, nahau
B. Semi, nahau
C. Chuku, semi
D. Tashhisi, tashibihi

**38.** Kwa nini wenzake Kaza hawakuonekana kuwa na hofu?

A. Walibahatika kuyahusudu mali yao kabla ya ubomoaji
B. Walikuwa wamezoea hali ya kuona na kushuhudia vibanda vikibomolewa
C. Hawakuwa na jingine la kufanya ila kuvumilia
D. Waliahidiwa kujengewa vibanda upya baada ya ubomoaji huo.

**39.** Si kweli kusema kuwa,

A. Kaza alishindwa kukabiliana na hali ya mjini
B. nyumbani kwa akina Kaza kulikuwa na shughuli zenye manufaa
C. Kaza hakunusuru chochote kabla ya kibanda kubomolewa
D. baridi ya asubuhi ilimpata Kaza nje alikokesha

**40.** Ni methali gani mwafaka kueleza kauli hii:
*Aliamua kufunganya virago vyake na kurudi nyumbani kushika jembe.*

A. Ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota mjini kuauniwa
B. Achanikaye kwenye mpini wa jembe hafi njaa
C. Mie nyumba ya udongo sihimili vishindo
D. Baada ya dhiki ni faraja

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

"Wawakilishi wa serikali yetu tukufu, wazee mliosheheni tajriba si haba, wazazi na vijana wenzangu hamjambo? Nimejawa na bashasha mpwitompwito kupata fursa hii adimu ili kuyaweka bayana masuala kadhaa kama mzalendo kindakindaki. Naomba usikivu wenu.

Waswahili husema kuwa mti hauendi ila kwa nyenzo. Nayo afya nzuri haimjii mtu tu. Afya hustahili kupaliliwa na kutunzwa kwa namna anuwai kama vile vyakula vyenye viinilishe, kufanya mazoezi na kuandama mienendo miadilifu. Usafi wa mwili na mazingira pia huchangia katika kuimarisha afya. Ni wazi kwamba mazingira yakiwa machafu hukosa kuvutia na kusababisha kuhanikiza kwa harufu **<u>inayokirihisha</u>**. Isitoshe, uchafu huwa hali mufti ya kuzaana kwa wadudu kama vile chawa, kunguni, nzi na mbu ambao ni maadui wakuu wa afya.

Kuna jambo ambalo hunishangaza mimi. Sijui kama wengine hushangaa ghaya ya kushangaa jinsi tulivyoshuka ngazi. Hebu pigeni darubini katika zama ambapo nchi jirani zililia ngoa kwa kuona nchi yetu ilivyopiga hatua. Walituona kama mfano wa kuigwa. Leo hii mambo ni tofauti; tumekuwa mumunye inayoharibikia ukubwani. Je, ni wapi tulipokanyaga chechele? Ni wapi tulipoenda segemnege? Ni kipi chanzo cha kibichi ikawa rangi ya hudhurungi?

Sisi kama wazalendo tunafaa tujifunge vibwebwe na kujikaza kisabuni ili kupambana na janga hili la umaskini. Taifa letu limekumbwa na shida tele za kiafya na mazingira jinsi nilivyotangulia kusema. Hata watalii hawalitembelei taifa letu tena. Je, serikali inafanya nini kurekebisha hali hii? Utalii ni kitegauchumi aaali kwa kuwa pesa za kigeni hutumika katika kuimarisha miundo duni. Miundo misingi hii huzalisha mali ya kuimarisha afya za raia wake. Serikali ili kuweza kuimarisha uwezo wake; yafaa kuimarisha mbuga za wanyama. Wengi watafanya kazi bungeni na kupata mkate wao wa kila siku. Hili litawezekana iwapo tutatunza mazingira, misitu na maliasili mengine.

Nchini Kenya, elimu ni mwangaza. Hata hivyo wengi wetu ni mbumbumbu wasioweza kuunganisha moja na moja kupata mbili. Katika siku hizi za mtandawezi, tutafanikiwa vipi bila elimu bora ikizingatiwa kuwa watoto wengi hawajawahi kutia mboni poa la darasa?Ni wajibu wa serikali kuzidisha shule za msingi na za upili hapa mashinani ili kuhakikisha watoto wengi wanapata elimu. Aidha, wanavyuo wahimizwe kufanya utafiti kwa ufadhili wa serikali ili kutoa suluhu ya matatizo tuliyonayo ya uvumbuzi.

Kando na hayo shughuli za ukulima zinafaa kuongezwa maradufu ili kupiga marufuku njaa, maradhi na umaskini. Kila familia inafaa kupata angalau kitu cha kutupa pangoni ili tusipukutiliwe machozi kupukupu kila tunapoona magazetini picha za vifyefye waliobaki magofu kutokana na njaa. Hili litafanyika ikiwa mbolea na mbegu zitatolewa kwa wakulima bila malipo ili waweze kujitosa kikamilifu katika kilimo.

Ufisadi umekita mizizi katika nchi yetu kiasi cha kuonekana kanuni na desturi. Kila uchao utasikia visa vya kunyimwa kazi kwa watu waliohitimu huku nafasi hizo zikitwaliwa na waliozunguka mbuyu ama walio na usuli mmoja na wakubwa. Je mtu aliyehongwa akipata kazi ataitekeleza kwa ari na mapenzi? Si matokeo yatakuwa kudhalilika kwa uchumi wetu?

Kwa kiasi kikubwa, uongozi bora unaadimika katika nchi yetu. Hatuna viongozi ila wanafiki. Wapiga kura wamekuwa wakijifaragua eti 'bora viongozi', na wala wasijue thamani ya viongozi bora. Je, hatukushuhudia uhasama, chuki na uchochezi kwa sababu ya siasa mbaya? Nao wawekezaji kutoka nchi za ng'ambo si walifunga virago nasi tukapoteza nafasi nyingi za kazi.

Fahari yetu hata hivyo haitarejea kwa ahadi za mmoja na lawama za waliosalia. Kidole kimoja hakivunji chawa. Aidha mkono mmoja hauchinji ng'ombe. Tunafaa kuungana kama umoja wa taifa moja na kutumia malighafi yetu vyema. Jambo kuu nililo nalo ni kumaliza umaskini wakati umefika wa kila mtu kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa. basi tufanye kazi kwa kutiana moyo bila ya kubaguana. Ziwe za juakali, biashara, ukulima, uhasibu au udereva angaa tufikie kilele cha mafanikio.

Wakati umefika wangu kulikunja jamvi kwa kuamba kuwa nia zikiwa pamoja kilicho mbali huja. Na nia tuko nazo. Mola awe nanyi daima dawamu."

41. Mzalendo kindakindaki ni
A. aliyezaliwa hapa nchini
B. anayehitajika hapa nchini
C. anayepatikana hapa nchini
D. anayethaminiwa hapa nchini

42. Maana ya **'Mti hauendi ila kwa uyenzo'** imejitokeza vipi katika aya ya pili?
A. Wanaokula vyakula vyenye viinilishe huzuia kunenepa
B. Wanaoepuka kazi hawapati shinikizo la damu.
C. Wanaozingatia mienendo mizuri hudumisha afya
D. Wanaonyoosha viungo vyao huwa wakakamavu

43. Kwa mujibu wa aya ya pili,
A. ni muhimu kutunza mazingira kwani tutarudisha hali ya kupendeza
B. ni muhimu kutunza mazingira kwani tutaepuka kuenea kwa harufu
C. ni muhimu kutunza mazingira kwani tutamaliza vikwazo tofauti vya afya.
D. ni muhimu kutunza mazingira kwani tutazuia ongezeko la wadudu waharibifu.

44. Mzungumzaji anadokeza kuwa
A. taifa lake limekuwa katika hali mbaya wakati wote
B. nchi yake imekuwa ikifuata mifano ya mataifa mengine
C. yeye binafsi haelewi chanzo cha matatizo yao
D. awali taifa lake lilikuwa katika hali nzuri kuliko sasa.

45. Maana ya **inayokirisha** ni
A. inayodhuru
B. inayoenea
C. inayoaibisha
D. inayochukiza

46. Manufaa ya utalii katika taifa ni
A. kuiletea nchi pesa za kigeni
B. kuzuri kwenye vivutio mbalimbali
C. kuiletea taifa utamaduni wa kigeni
D. kutunza mazingira, msitu na maliasili mengine

47. Ili kuhakikisha watoto wanapata elimu, yote haya ni muhimu ila
A. utafiti ufanyike kutoa suluhu kwa matatizo
B. shule zifadhili utafiti wa kuchunguza matatizo
C. serikali iongeze shule katika maeneo mbalimbali
D. wanavyuo wafanye utafiti ili kutoa suluhu

48. Madhara ya ufisadi yaliyoangaziwa kwenye makala haya ni pamoja na
A. watu waliohitimu kupata nafasi za kazi
B. kudhalilisha utendakazi na kuathiri uchumi
C. uchefuchefu wa kazi kwa wote mafisadi
D. kupatikana kwa viongozi wanafiki katika taifa

49. Elimu ni mwangaza. Hii ni tamathali gani ya lugha?
A. Istiari
B. Tashbihi
C. Ishara
D. Chuku

50. Picha zinazoonekana magazetini zinahusu,
A. miradi mbalimbali ya kilimo
B. maeneo yanayokauka kwa makali ya ukame
C. watu waliokondeana kwa makali ya njaa
D. Watu wanaopukutikwa na machozi kwa makali ya njaa